TANGAZO LA SERIKALI NA. 549 la tarehe 26 Jul 2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA YA 272)

**AMRI**

*(ImetolewakwamujibuwaKifungu Na.28(1)(d))*

AMRI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MUHEZA (“MUHEZA WSSA”), LA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2019

Kichwa cha Amri

1. Amri hii itajulikana kama, Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Muheza (“Muheza WSSA”), (la Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira), la Mwaka 2019

Tarehe ya kuanza utumika

2. Amri hii itachukuliwa imeanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Julai 2019.

Marekebishoya bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Muheza WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) Muheza WSSA kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Agizo hili.

(b) Muheza WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii.

(c) Muheza WSSA itazingatia kifungu cha 43 cha Sheriaya EWURA, Sura namba 414 na kifungu

cha 6 ya Kanuni za EWURA za Taratibu za Ukusanyaji wa Ada na Tozo zilizochapishwa katika Gazeti la Serikali namba 193 za mwaka 2010.

(d) Kabla ya tarehe 1 Oktoba 2019, Muheza WSSA itawasilisha Mpango wa Biashara uliorekebishwa ambao unahusisha bei iliyoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Kanuni hii.

(e) Muheza WSSA itahakikisha ripoti zake za kifedha zinakaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) au taasisi yeyote ya ukaguzi wa fedha iliyoidhinishwa kama kifungu cha 33 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma na kupeleka nakala za taarifa za kifedha zilizokaguliwa kwa EWURA.

(f) Muheza WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri za Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne la Amri hii.

Amri Na. 11-014 la trehe 1 Juni 2011

5. Amri hii linasitisha matumizi ya Amri Na. 11-014 katika maeneo yanayohudumi wa na mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Muheza (Muheza WSSA).

**MAJEDWALI**

## JEDWALI LA KWANZA

*(Imetengenezwa chini ya Aya ya 3)*

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1.1: Bei za Maji za Sasa, Zilizopendekezwa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi / MitayaUjazo)

| Wateja | Matumizi | Bei za Sasa | Bei Zilizopendekezwa | | | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 0-10 | 450 | 1,390 | 1,410 | 1,450 | 1,100 | 1,150 | 1,200 |
| | >10 | 495 | 1,530 | 1,550 | 1,590 | 1,200 | 1,250 | 1,300 |
| Biashara | | 510 | 1,570 | 1,650 | 1,700 | 1,300 | 1,400 | 1,400 |
| Taasisi | | 500 | 1,540 | 1,560 | 1,620 | 1,300 | 1,300 | 1,300 |
| Viwanda | | 500 | 1,700 | 1,720 | 1,770 | 1,400 | 1,400 | 1,400 |
| Kioski | | 500 | 1,500 | 1,500 | 1,500 | 1,000 | 1,000 | 1,000 |

Jedwali Namba 1.2: Bei za Maji za Sasa, Zilizopendekezwa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja WasionaDira

| Wateja | Bei za Sasa | Bei Zilizopendekezwa | | | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 4,500 | 15,300 | NA | NA | 10,000 | 10,000 | NA |
| Taasisi | 9,500 | 28,260 | NA | NA | NA | NA | NA |
| Biashara | 10,000 | 30,800 | NA | NA | NA | NA | NA |
| Viwanda | 13,000 | 42,500 | NA | NA | NA | NA | NA |

JedwaliNamba 1.3: Tozo za Sasa, Zilizopendekezwa na Zilizoidhinishwa za gharama ya huduma

| Wateja | Tozo za Sasa | Bei Zilizopendekezwa | | | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 500 | | | | | | |
| Taasisi | 500 | | Haihitajiki | | | Haihitajiki | |
| Biashara | 500 | | | | | | |
| Viwanda | 500 | | | | | | |

JedwaliNamba 1.4: Ada za Sasa, Zilizopendekezwa na Zilizoidhinishwa kwa kila Maunganisho Mapya ya Maji.

| Wateja | Ada za Sasa | Bei Zilizopendekezwa | | | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 160,000 | | | | | | |
| Taasisi | 160,000 | | | | | | |
| Biashara | 160,000 | Asilimia 20 ya matumizi yanayotumika kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 24 cha Kanuni za Maji, 2013 | | | Asilimia 20 ya matumizi yanayotumika kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 24 cha Kanuni za Maji, 2013 | | |
| Viwanda | 160,000 | | | | | | |

JedwaliNamba 1.5 : Tozo za Sasa, Zilizopendekezwa na Zilizoidhinishwa kwa kila Marejesho ya huduma ya Maji.

| Wateja | Tozo za Sasa | Bei Zilizopendekezwa | | | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Majumbani | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 | 10,000 |
| Taasisi | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Biashara | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Viwanda | 10,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |

## JEDWALI LA PILI

*(Imetengenezwa chini ya Aya ya 4(a))*

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA

| MaelezoyaUwekezaji | Kipindi cha Utekelezaji (TZS '000,000) | | |
|---|---|---|---|
| | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Ununuzi na uweke mita 1,330 za maji ya wateja kwa wateja wasio na mita | 86.30 | 26.75 | - |
| Ununuzi na uwekaji programu ya bili Juni 2022 | - | - | 20.00 |
| Ununuzi wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa eneo la kumwaga sludge | - | 7.50 | 7.50 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ununuzi wa vifaa vya ukaguzi na zana zingine za kufanyakazi. | - | 3.00 | 3.00 |
| Ununuzi wa thamani za ofisi | - | 3.00 | 3.00 |
| Ununuzi wa Komputa 3 na printamoja | - | 10.00 | 12.50 |
| Ununuzi wa mashine (3) za kutoa kopi | - | 10.00 | 11.00 |
| Ununuzi wa pikipiki tatu | - | 3.00 | 6.00 |
| Jumla ya gharama y auwekezaji | 86.30 | 63.25 | 63.00 |
| | | | |
| MaelezoyaUkarabati | | | |
| Ukarabati wa chemba mbili zilivyopo eneo la Mkulumuzi | - | - | 5.00 |
| Ukarabati eneo la kilomita 5 la mtandao wa usambazaji wa maji ambao umechakaa sana. | - | 94.58 | 94.58 |
| Ununuzi na kufunga mita 300 za maji ili kubadilisha mita za zamani na zilizoharibika | - | 12.75 | 12.75 |
| Ununuzi na kufunga mita kubwa 7 ili kubadilisha mita za sasa | - | 2.25 | 2.25 |
| Kupiga plasta na kubadilisha mifuniko y achuma | - | 0.70 | 0.70 |
| Kubadili bomba la kusambaza maji Km 10, valvu 20na ukarabati wa valvu za chemba | - | 47.29 | 47.29 |
| Ukarabati Km 2 eneo la chanzo cha Mkulunzi | - | 75.66 | - |
| Ujenzi wa fensi eneo la pampu iliyopo sokoni na ukarabati wa jengo la ofisi | - | 3.50 | - |
| Ununuzi na ukarabati wa thamani za ofisi | - | 10.00 | 13.00 |
| Ununuzi wa Pikipiki mbili ili kubadilisha za sasa | - | 3.00 | 8.00 |
| Ununuzi wa Komputer tatu ili kubadilisha za sasa | - | 5.13 | 2.76 |
| Jumla ya gharama ya Ukarabati | - | 254.85 | 186.32 |
| Jumla kuu ya gharama ya Uwekezaji na ukarabati | 86.30 | 318.10 | 249.32 |

## JEDWALI LA TATU

*Imetengenezwa chini ya Aya ya 3)*

VIASHIRIA VYA UTENDAJI

| Maelezo | Kipimo | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Watu wanao pata huduma ya maji | % | 75 | 78 | 82 |
| Kiwango cha upotevu wa maji | % | 45 | 40 | 35 |
| Wateja wenye dira za maji | % | 80 | 100 | 100 |
| Ufanisi ukusanyaji mapato ya mwaka husika | % | 92 | 94 | 95 |
| Kiwango cha kukidhi ubora wa maji (E-coli ) | % | 100 | 100 | 100 |
| Kiwango cha kukidhi ubora wa maji (Turbidity ) | % | 60 | 70 | 80 |
| Wastani wa saa za huduma | Saa | 12 | 12 | 12 |

## JEDWALI LA NNE

*Imetengenezwa chini ya Aya ya 4(f))*

Mahitaji ya Mapato (Milioni TZS)

| Maelezo / Mwaka | Gharama zilizoidhinishwa (Milioni TZS) | | |
|---|---|---|---|
| | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 |
| Gharama ya uendeshaji | 707.50 | 971.08 | 993.64 |
| uchakavu | 104.34 | 89.90 | 101.94 |
| Kufidia Uwekezaji | 73.71 | 84.28 | 73.86 |
| Mahitaji ya Mapato | 885.55 | 1,145.25 | 1,169.44 |
| Ondoa | | | |
| Mapato mengine | 37.79 | 38.35 | 40.21 |
| Mapato ya mauzo ya maji | 847.76 | 1,106.90 | 1,129.22 |

Dodoma
.............................. 2019

NZINYANGWA E. MCHANY
*Mkurugenzi Mkuu*